MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA

JARIDA LA HALI YA HEWA KILIMO

Na. 02: Msimu wa Kilimo 2021/2022 *Tathmini ya Oktoba 1-10, 2021 na Matazamio Kipindi cha Oktoba 11-20, 2021*

MUHTASARI

- Hali ya ukavu inayotarajiwa inaweza kuathiri upatikanaji wa maji na malisho kwa mifugo.
- Mvua zinazotarajiwa kwa baadhi ya maeneo nchini hususan nyanda za juu kaskazini mashariki na pwani ya kaskazini zinaweza kufuatiwa na vipindi virefu vya ukavu na kuathiri uoteshaji wa mazao

MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA OKTOBA 1-10, 2021

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa Ikweta (St.Helena na Mascarene) iliendelea kuwa na mabadiliko kidogo wakati ile iliyopo kaskazini (Azores na Siberia) ilipungua nguvu kidogo. Hali hii iliendelea kusababisha upepo wenye nguvu ya wastani kuvuma kutoka kusini mashariki kuelekea maeneo ya pwani ya bahari ya Hindi. Joto la bahari lilikuwa juu kidogo ya wastani maeneo ya mashariki mwa bahari ya Hindi wakati magharibi mwa bahari hiyo lilikuwa la wastani. Hali hii ilisababisha kuwa na mchango mdogo katika kuusukuma upepo wenye unyevunyevu kuvuma kuelekea maeneo ya ukanda wa pwani na hivyo kusababisha vipindi vichache vya mvua nyepesi katika maeneo hayo. Mifumo hii ya hali ya hewa, iliendelea kusababisha maeneo mengi ya nchi kuendelea kuwa makavu isipokuwa maeneo machache ya ukanda wa pwani ambayo yaliendelea kupata mvua nyepesi pamoja na maeneo ya ziwa Victoria na maeneo machache ya magharibi mwa nchi ambayo yaliendelea kupata vipindi vifupi vya mvua zilizoambatana na ngurumo za radi.

MWENENDO WA MVUA KATIKA KIPINDI CHA OKTOBA 01-10, 2021

Kwa ujumla, maeneo mengi nchini yalikuwa makavu isipokuwa maeneo machache ya ukanda wa pwani na mikoa ya Mara, Simiyu, Mwanza, Geita, Arusha, Manyara, Kilimanjaro, Kigoma,Tabora, Rukwa, Katavi na Songwe ambayo yamepata mvua chache kama inavyoonekana katika Kielelezo.



Kielelezo 1: Kiasi cha mvua kwa kipindi cha Oktoba 1-10, 2021

TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA OKTOBA 1-10, 2021

Katika dekadi ya kwanza ya mwezi Oktoba, wakulima katika maeneo yanayopata mvua mara mbili kwa mwaka waliendelea na shughuli za maandalizi ya mashamba kwa ajili ya msimu wa mvua za vuli isipokuwa katika mikoa ya Kagera na Mara ambako baadhi ya wakulima wameendelea kupanda mahindi, maharagwe na mhogo kwa kutumia mvua chache zilizonyesha katika maeneo hayo. Hata hivyo, baadhi ya mazao katika mkoa wa Kagera yameripotiwa kuathirika kutokana na vipindi virefu vya ukavu.

Kwa maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka baadhi ya wakulima waliendelea na

uandaaji wa mashamba kwa ajili ya mvua za msimu.

Maji na malisho ya mifugo viliendelea kupungua katika maeneo mengi nchini kutokana na hali ya ukavu inavoendelea.

HALI YA MAJI KATIKA KIPINDI CHA OKTOBA 1-10, 2021

Katika dikadi hii, kina cha maji katika mabwawa, mabonde na mtiririko wa maji kwenye mito viliendelea kupungua kutokana na hali ya ukavu iliyoendelea katika maeneo mengi nchini.

MIFUMO YA HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA OKTOBA 11-20, 2021

Katika kipindi hiki cha dikadi, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini inatarajiwa kupungua nguvu kidogo wakati ile iliyopo kaskazini ikitarajiwa kuimarika kidogo. Hali hii inatarajiwa kuendelea kusababisha upepo wenye nguvu ya wastani kuvuma kutoka kusini mashariki kuelekea maeneo ya pwani ya bahari ya Hindi. Joto la bahari la juu kidogo ya wastani linatarajiwa upande wa mashariki mwa bahari ya Hindi wakati magharibi mwa bahari ya Hindi joto la bahari linatarajiwa kuwa la wastani. Hali hii inatarajiwa kuwa na mchango mdogo katika kuusukuma upepo wenye unyevunyevu kuvuma kuelekea maeneo ya ukanda wa pwani. Kwa ujumla, mifumo hii ya hali ya hewa inatarajiwa kusababisha maeneo mengi ya nchi kuendelea kuwa makavu isipokuwa maeneo machache ya ukanda wa pwani ambayo yanatarajiwa kupata mvua nyepesi pamoja na maeneo ya kanda ya ziwa Victoria na maeneo machache ya magharibi mwa nchi ambayo yanatarajiwa kuendelea kupata vipindi vifupi vya mvua zitakazoambatana na ngurumo za radi.

HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA OKTOBA 11-20, 2021

Maeneo ya kanda ya Ziwa Victoria (mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara) pamoja na magharibi mwa nchi (mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora) yanatarajiwa kupata vipindi vifupi vya mvua na ngurumo za radi katika maeneo machache.

Nyanda za juu kaskazini mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro) pamoja na pwani ya kusini (mikoa ya Mtwara na Lindi yanatarajiwa kuwa makavu kwa ujumla na yenye vipindi vichache vya mvua nyepesi.

Pwaniya kaskazini (mikoa ya Tanga, maeneo ya kaskazini mwa Morooro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba pamoja na yanatarajiwa kupata vipindi vifupi vya mvua nyepesi katika maeneo machache.

Maeno ya nyanda za juu kusini magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa), mikoa ya kusini (Ruvuma na kusini mwa Morogoro) pamoja na kanda ya kati (mikoa ya Dodoma na Singida) yanatarajiwa kuwa makavu kwa ujumala.

HALI YA HEWA KILIMO: MATARAJIO NA USHAURI KIPINDI CHA OKTOBA 11-20, 2021

Mvua zinazotarajiwa kwa maeneo ya ukanda wa pwani pamoja na nyanda za juu kaskazini mashariki zinaweza kufuatana na vipindi virefu vya ukavu na kuathiri uoteshaji wa mazao katika maeneo hayo.

Pia, hali ya ukavu inayotarajiwa inaweza kuathiri upatikanaji wa maji na malisho kwa ajili ya mifugo.

Wakulima, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kupata ushauri zaidi kutoka kwa wataalamu wa sekta husika. Pia, inashauriwa kuendelea kufuatilia utabiri wa hali ya hewa wa kila siku, siku tano na tahadhari kadri zinavyotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania nchini (TMA).

HALI YA MAJI INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA OKTOBA 11-20, 2021

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kuendelea kupungua katika maeneo mengi nchini kutokana na hali ya ukavu inayotarajiwa. Hivyo, wananchi na mamlaka husika wanashauriwa kutumia rasilimali maji kwa uangalifu.

Jarida limetayarishwa na:
Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania
Ghorofa ya 3 -Ubungo Plaza – 388 Barabara ya Morogoro,
S.L.P 3056; 16102 Dar es Salaam, Simu. 255 -(0) 22 – 2460706-8; Nukushi: 255 - (0) 22 – 2460718 ; Barua pepe: (1) met@meteo.go.tz (2) agromet@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz, Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania